

KWA NINI BETHLEHEMU MDOGO?

 Inaweza ionekane kwa namna fulani inachekesha, asubuhi hii, kuvaa kabuti langu jukwaani, bali nilifurahia sana ku—kuonyesha hilo kabuti zuri nililopewa na kanisa hili. Nilimuona Ndugu Neville hapa juzijuzi, amevaa ile suti ya kupendeza, jinsi ilivyomkaa vizuri mno, na nikawaza, vema, ni. . . Ilionekana nzuri mno, na kusanyiko langu linazungumzia habari zake, nikafikiri, “Nitavaa tu kabuti jukwaani.”

² Unajua, ninaamini kamwe hatukui. Sikuzote tu. . . Nami sitaki kukua. Unalionaje hilo, Ndugu Luther? La, kamwe hatutaki kukua, tunapenda siku zote tu kudumu tukali watoto.

³ [Ndugu Neville anasema, “Ndugu Branham, nilidhani ulikuwa umevaa moja ya mavazi yale kama hawa wahudumu wa tabaka ya juu zaidi. Nilikukonyeza jicho upande, nami nikafikiria labda umevalia joho.” Ndugu Branham na kusanyiko wanacheka—Mh.] Hongera kwa kabuti hilo zuri.

⁴ Vema, nitasema ni—ni. . . Nilihitaji moja sana, na ni zuri sana kuliko lo lote nililowahi kuwa nalo. Nami hakika nalipenda. Na Ndugu Roy Roberson, sijui yupo hapa asubuhi hii au la, alihusika na kulichagua. Na lilikuwa chaguo zuri hasa, nasi tuna—tuna—tunafurahia sana kuzipata.

⁵ Na kwa hiyo tunafurahi sana kurejea katika nyumbani ya Mungu aliye hai, asubuhi hii, na kufurahia nyakati hizi za ajabu za—za ushirika kwenye Neno Lake la thamani.

⁶ Na nimekaribia sasa, Bwana akipenda, yanibidi niende ng’ambo. Na nafikiri mmeliona katika *Sauti* ya Wafanyi Biashara, kwamba ninaondoka kwenda ng’ambo mwezi huu ujao. Nasi tutayataka sana maombi yote ya watu, kwamba watatuombea wakati tuondokapo. Inaelekea kwamba huko ng’ambo mikutano yangu yaelekea kuwa mizuri zaidi, kwa sababu inakuwa mizuri zaidi huko. Marekani. . .

⁷ Nilikuwa ninamwambia Ndugu Mercier ambaye nilimsikiliza. . . Alinipa gramafoni, kwanza, na ilikuwa na sahani za santuri, za baadhi ya mahubiri yangu. Hapo nikajua, kama mtu ye yote atawahi kunisikiliza, ingebidi iwe ni neema ya Mungu kwao, kwa sababu nilifikiria ningeweza kufanya vizuri zaidi kidogo.

⁸ Yeye anazinasu, pia. Ki—kidogo, unaweza kukata kisehemu hicho, unaona. Au, anashikilia chini kidole chake cha gumba, nadhani huko ni kukata.

⁹ Bali na—nawaambieni, nilishangazwa sana. Mimi. . . Mahubiri mabaya sana niliyowahi kusikia maishani mwangu, yalikuwa ni yangu mimi, hilo ni kweli, kwenye—kwenye—kwenye

sahani ya santuri. Mimi...Ilinifanya niwe na fadhaa sana, sikuweza hata kula chakula changu cha mchana. Niliugua, nikaondoka mezani, sikuweza kulala usiku ule.

¹⁰ Nami nikashuka kwenda huko Kentucky, pamoja na Ndugu Wood jana. Wakati niliporudi, nilisema, “Ndugu Wood, sioni jinsi ambavyo nitawahi kumfanya mtu ye yote aje kunisikiliza nikizungumza. Ni mbaya m—mno, kujirudiarudia mwenyewe, na, loo, hamna ufasaha wa lugha, na, vituo, hamna—hamna vyo vyote.” Mimi kwanza...sijui. Nikasema, “Ilinitia moyo kwa njia moja, kujua lazima iwe ni Mungu, au hakuna mtu ye yote angekuja kamwe.” Hilo ni sawa.

¹¹ Kwa hiyo nilikuwa ninazungumza na Ndugu Collins. Nadhani yumo humu jengoni. Na kwa hiyo nikamwambia... Akaja, nami nilikuwa nikimwambia kuhusu hilo. Nikasema, “Ndugu Collins, mimi kwa kweli...” Nikasema, “Nimekaribia kabisa miaka thelathini, kama mhubiri, nami hakika yanipasa nijue mahubiri ni nini.” Nikasema, “Hayo ndiyo mabaya kuliko yote niliyowahi kuyasikia.”

¹² Naye—yeye ni mhudumu wa Kimethodisti, na ndugu yake ni mtu kweli katika dhehebu la Kimethodisti. Naye akasema, “Vema,” akasema, “nitakwambia, Ndugu Branham,” kasema, “huenda hivyo vituo na—na sentensi zako visiishie kwa ufasaha, na mambo kama hayo, bali,” kasema, “uliwahi kufikiria kuhusu yule jamaa ambaye alihubiri Siku ya Pentekoste, ambaye hakuweza hata kuandika jina—jina lake mwenyewe, jina lake Petro?” Kasema, “Ninawazia huo haukuwekewa vituo sawasawa.”

¹³ Lakini, unaona, kinachomfanya mtu kuangalia hayo, mnasikiliza haya matangazo haya ya radio, na hayo yote yameandikwa, mnaona. Nao wao—wao wanaweza kuuandika na kuuwekea vituo, na kadhalika kwa sababu wanausoma.

¹⁴ Nilisimama pamoja na Charles Fuller, nikihubiri nyuma ya hori lililokuwa namna *hii*, kwa jukwaa lake. Na kila kitu alichonena, alikisoma chote, namba moja, namba mbili, namba tatu, namba nne, namna hiyo, mpaka alipoumaliza wote, na kuuwekea muda. Na wote ulikuwa umekaguliwa, umekaguliwa kwa ajili ya radio, na kila kitu.

¹⁵ Kwa sababu, naye Billy Graham, niliona wake, na kadhalika, ambapo wao husimama tu hapo na kuuzungumza, huusoma tu haraka wawezavyo, na wote uko tayari, kwa hiyo nadhani ungepata vituo.

¹⁶ Lakini shida yangu, singeliweza hata kuusoma. Kwa hiyo, na kama ningeuandika, nina hakika nisingeweza kuusoma. Kwa hiyo ni neema ya ajabu, sivyo, kuona ambalo Yeye aweza kututendea. Lakini ninashukuru kuanza hivi sasa, kumalizika kwa mwaka huu uliokwisha, kuanza mwaka mpya.

¹⁷ Nilisikiliza mstari wa maombi, na hakika sikuridhishwa na mstari ule wa maombi, pia, kuusikiliza. Ni mara ya kwanza nimewahi kujisikiliza mwenyewe namna hiyo, kwa—kwa ujumbe, nami hakika nilishangazwa, mistari ya maombi haiendi ipaswavyo. La, nafikiri itakuwa kwamba, baada ya kitambo kidogo, itakuwa kwamba kila mtu atapaswa ajue kila kitu kuhusu wao kabla ya wao kuamini. Na kuanzia mwanzoni mwa mwaka, nataka kubadili hilo, na kuanza tu mstari wa maombi po pote Mungu anenapo nami, “mtu *huyu* yupo nje ya mstari,” au jambo fulani lisilo sahihi, nitakomea kwa huyo. Kuwaacha waliobakia wapite, sababu huwapishi wengi kutosha namna hiyo, unaona. Watu hujua walipo, na wao ni nani, na walilotenda. Lakini wanaona kitu ambacho hakipatani vilivyo na Mungu, huo ndio wakati wa kukomea kwa huyo, tuseme, “*huyu* ndiye,” unaona. Kwa hiyo nafikiri labda kutakuwa na baadhi ya mabadiliko yatakayofanyika, Ndugu Leo, tangu nilipozisikia, nami natumaini kwamba Mungu atatusaidia katika mwaka ujao.

¹⁸ Sasa, naamini kwamba usiku wa leo wana ibada hapa Maskanini. Na mimi yanipasa niwe hapa katika 62, pamoja na Ndugu Ruddell, usiku wa leo. Nasikia kwamba watafanya ibada ya mkesha hapa. Na Ndugu Ruddell alinialika kwenye ibada ile ya mkesha, lakini nikiwazia labda ningerudi kwenye Maskani, mnamo usiku ule, kwa sababu sikuzote nimejaribu kuwa Maskanini kwenye—kwenye usiku unaotangulia mwaka mpya, nami nilitaka kushuka nje hapa na ndugu hawa hapa. Kwa hiyo kwa namna fulani nilipatana kidogo, nami nitakuwa pamoja na Ndugu Ruddell usiku wa leo, nje kwenye 62, kwenye Klabu cha kale cha 62 ambacho kimebadilishwa kuwa ka—kanisa. Na halafu Jumatano usiku tutarudi hapa kwenye ibada ya mkesha. Ndiposa Alhamisi tunaondoka kuelekea Chicago, kisha tuendelee hadi Philadelphia, na kisha ng’ambo.

¹⁹ Na asubuhi hii, hatutaki kuwachelewesha sana, kwa sababu ni . . . tuna mahojiano, na ibada zinaendelea.

²⁰ Na, tuseme, tangu ibada ya mwisho ya maombi hapa, loo, ninashukuru sana kwa matokeo ambayo yalitokana na ibada ya mwisho ya maombi. Ilikuwa kweli jambo la ajabu ambalo Bwana anaweza kutenda watu Wake wanapokusanyika pamoja. “Wao ambao wana . . . wataliita Jina la Bwana, wakusanyike pamoja,” naamini ndivyo ilivyo, “na—na kuomba, basi Mungu atasikia kutoka Mbinguni.”

²¹ Kwa hiyo na tuinamishe vichwa vyetu, muda kidogo sasa, tunapomtazamia Yeye kutupa uvuvio unaohitajika kwa Ujumbe huu.

²² Bwana, Wewe umekuwa kimbilio letu na nguvu zetu katika vizazi vyote. Mababa zetu, mbele zetu, walikutumainia Wewe, nao hawakuaibika. Waliliamini Jina Lako Takatifu, nao

wakatokezwa kama nuru zing'aazo; na sisi tukiwaangalia, kama mshairi alivyosema, "Nyayo juu ya mchanga wa wakati; kuachana kwetu huziacha nyuma yetu, nyayo katika mchanga wa wakati." Kisha tunaona kwamba wale ambao wamekutumainia Wewe, sikuzote, bila ya kushindwa wakati mmoja, wanafanikiwa. Ingawa wamepitia maji mengi yenye kina kirefu na—na majaribu makubwa na mateso, lakini hata hivyo, mwishowe, Wewe sikuzote uliwatoa "zaidi ya washindi," kwa sababu ni Neno Lako lililoahidiwa kwamba Wewe ungetenda hili.

²³ Basi tungeomba, leo, kwamba ungebariki kanisa hili dogo. Mbariki mchungaji wake, ndugu yetu mzuri, Ndugu Neville, na familia yake. Tunaomba kwamba Wewe utakuwa tu pamoja naye katika mwaka ujao, na utamtia upako kwa nguvu zaidi na—na kumbariki katika kila njia. Tia nguvu afya ya familia yake, watoto wadogo ambao wanakua. Mdumishe imara na katika afya Ndugu Neville.

²⁴ Na bariki kanisa hili na kila mshirika aliyeko ndani yake. Halmashauri ya wadhamini, jinsi tunavyowapenda kama watu hodari sana wa Mungu; na halmashauri ya mashemasi, wao pia ni watumishi Wako hodari. Na watu wote wanaokuja hapa, tunashukuru kwa ajili yao, Bwana. Inanitia tu nguvu moyoni mwangu kujua kwamba kidimbwi hiki kidogo cha siku nyingi na kishemu chenyewe majani kilicho pembeni, miaka mingi iliyopita, kimefanywa mnara wenye taa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Nami naomba, Mungu, kwamba utadumu hata Yesu ajapo. Na watu wengi mashuhuri ambao wamekuwa hapa, Bwana, watokeze Siku ile, wakiwa wameoshwa katika Damu ya Mwana-kondoo. Wajalie.

²⁵ Na tunapofungua hili Neno Lako lililobarikiwa, asubuhi hii, Bwana, kwa kugeuza kurasa ili kusoma kutoka Humo fungu la maneno, nasi tunajua kwamba Wewe peke Yako Ndiwe uwezaye kutoa somo. Nasi tunaomba, Mungu, kwamba Wewe utalitia upako Neno Lako, na jalia liende moja kwa moja kwenye mioyo ya watu likawafaidi. Fanya waamini toka katika wasioamini; na watie nguvu Wakristo; na uwaponye wagonjwa; na wape moyo waliovunjika moyo; na ujiipatie utukufu kwa Nafsi Yako. Ili kutenda hili, Bwana, tahiri midomo itakayonena na masikio yatakayosikia. Kwani twaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

²⁶ Nikitangaza kifungu kidogo ambacho ni...kilishuka moyoni mwangu tangu Jumapili iliyopita. Nami nilikuwa nikizungumzia juu ya wale mamajusi wakija kwa—kumuona Yesu, ile Nyota waliyoifuatia toka Mashariki hata Magharibi; wakati najifunza hilo, nilipata Andiko, na kisha sikupata kuwa hapa siku iliyotangulia Krismasi kwa sababu ya ibada za jela, na kadhalika, nilikopaswa kuwa. Nilifikiria ningezungumzia leo juu ya somo la: *Mbona Bethlehemu Mdogo?*

27 Nami nataka kusoma kutoka katika Kitabu cha Mika, nabii, mmoja wa manabii wadogo, sura ya 5 na aya ya 2. Inasema hivi.

Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka...kutoka kwako wewe...atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala... atakayekuwa mtawala katika Israel; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamami za kale, tangu milele.

28 Nalikuwa na doa katika Andiko pale, ndiyo sababu sikufahamu lilikuwa neno gani, wakati ule.

29 Kati ya mahali po pote palipo Palestina! Na humo mna miji mingi mikubwa, na mitaa yake, na miji mikubwa ambayo inaelekea inajulikana zaidi katika elimu ya historia, na kuzingirwa kwa ngome vizuri zaidi, miji mikubwa zaidi. Basi kwa nini Mungu angechagua Bethlehemu mdogo kuwa mahali pa kuzaliwa Mwanawe? Kuna mingi ambayo ni mikubwa zaidi. Na kwa mfano, elimu ya kihistoria ya Yerusalemu, Yerusalemu wenye kiburi, mji mkuu wa nchi nzima, na ni mmoja wa miji mikubwa kuliko yote ya Palestina. Na basi twashangaa kwa nini Mungu angechukua hicho kijiji kidogo cha Bethlehemu, kuwa mahali pa kuzaliwa Mwanawe.

30 Lakini kama Maandiko yalivyonena, “Kile Mungu amekusudia kutenda, kitatendeka.” Na kuna Mungu, aliyekikusudia kiwe hivyo tangu awali au hakingekuwa hivyo kamwe. Na hapo Maandiko yanasema, katika sura ya 15 ya Matendo, kwamba, “Hakuna jambo la bahati.” Mungu alijua kila kitu. Na haikutokea kutendeka namna hiyo. Ilikuwa tu kwamba Mungu akifanya jinsi hiyo.

31 Na basi wakati sisi katika akili zetu zenye kikomo tunaanza kufikiria, “Kwa nini Mfalme mkuu wa Mbinguni angechagua mahali padogo kama hapo, badala ya mji mkuu?” Badala ya baadhi...

32 Hata kulikuwa na sehemu nyingi ambazo zimekuwa na mazingira makubwa ya kiroho kuliko ulivyokuwa Bethlehemu. Kwa mfano, baadhi ya mahali kama Shilo. Shilo palikuwa mahali pa kale walipoabudia Israeli, ambapo wote walikuja mwaka baada ya mwaka mahali hapa pakuu ambapo lile sanduku la agano la Bwana liliwekwa. Nami nashangaa kwa nini, basi, kwamba Yeye asingezaliwa hapo Shilo?

33 Kisha kulikuwa na Gilgali, mahali pengine maarufu pa kiroho pa kuabudia. Kwa nini basi Mungu asingemwacha azaliwe hapo Gilgali?

34 Na kulikuwepo na mwingine, Sayuni. Sayuni ulikuwa juu ya kilele cha mlima. Nasi twashangaa kwa nini basi Yesu asingezaliwa basi katika Sayuni, kwa sababu pamekuwa alama kubwa ya kihistoria ya mahali ambapo Bwana amebariki watu Wake kwa miaka mingi.

35 Na inaonekana kama kwamba labda Yeye angechagua Sayuni, au Gilgali, au—au Shilo, au moja ya mahali pengine pakuu ambapo pamekuwa na baraka kuu na mafundisho makuu.

36 Na kulikuwa na miji mingine mikubwa, kama vile Hebroni. Hapo ndipo palikuwa mahali kwa mtu anayetaka mji wa kimbilio, mahali pa usalama. Kulikuwa na Ramothi iliyo Gileadi, pia, mahali pengine pa kimbilio ambapo watu wangeweza kuja, ambao ungelifaa sana Kwake kuzaliwa.

37 Na pengine, kama ninge kuwa nikilifikiria hilo, ningemleta Yeye hapo Kadeshi-barnea kwani hapo palikuwa na kiti cha hukumu, na mahali pa kukimbilia. Labda ningelimleta Yeye hadi nchi ile mahali pa kuzaliwa Kwake, au labda tungelichagua baadhi ya hiyo miji mingine.

38 Lakini, unajua, ninafurahia sana kwamba hata mambo madogo yasiyo na uzito katika Biblia yana maana sana. Naamini kwamba Yesu ndiye aliyesema hili, kwamba, “Mnaepa, na kutenda mambo makuu ya sheria,” hasa, “lakini mwayaacha mambo madogo.” Na wakati mwingine mambo madogo madogo ndiyo yanayoshikamanisha mambo makubwa. Lakini, basi, meno makuu ya gurudumu yanazunguka sawa kabisa na vile Mungu alivyoyakusudia tangu awali kufanya. Geuza hapa, kamwe hapatakuwa na moja litakalokosea mahali pake. Mungu amekwisha kukusudia awali mambo yote, na lazima ligonge sawa sawa tu kwenye mahali pale.

39 Nasi tupatapo imani kama hiyo, na kuanza kufikiria juu ya, “Nani aliye nyuma ya haya yote haya? Ni springi gani kuu ambayo inaendesha uchumi huu mkuu wa Mungu?” Tunaona ni Roho Mtakatifu. Haikuachwa katika mikono ya binadamu kufanya mambo; bali katika mikono ya Roho Mtakatifu. Naye ndiye springi iliyo kuu, kwamba kama anaweza kupata vyombo vile vingine vyote, kazi itatendeka kikamilifu na kudumisha wakati wa Mungu barabara.

40 Na kisha tunaona hayo na tunashangaa niani mwetu basi, tuangaliapo mambo makubwa na jinsi ambavyo tungeyapata; na kisha inatupa faraja nyingi leo kufikiria kwamba, labda kama tu kundi dogo la watu, labda kama sisi ni watu duni kwa ulimwengu na kwa makanisa makubwa ya madhehebu, hata hivyo Mungu hutumia mambo hayo madogo na rahisi wakati mwingine.

41 Kwa maana imeandikwa pia katika Maandiko, “Msiogope, enyi kundi dogo, ni mapenzi ya Baba yenu kuwapa ule Ufalme.” Ni faraja ya jinsi gani, kwamba, najua kwamba kwa hakika tu kama ilivyompasa Yesu kuzaliwa katika Bethlehemu mdogo, hivyo kundi lililo dogo ndilo ambalo Baba atalipa Ufalme, kwa sababu imeandikwa. Na Maandiko yote yana pumzi ya Mungu, nayo Maandiko hayawezi kuvunjwa. Lazima yatimizwe. Kwa

hiyo inatupa lile tumaini, kujua kwamba—kwamba itakuwa ni kundi dogo ambalo litapokea Ufalme, kundi dogo la waaminio waaminifu. Ninatumainia kuwa mmoja wa kundi hilo, au, kuwa katika kundi hilo dogo, ningesema.

⁴² Na basi tunajua ile hadithi, wengi wetu wanafahamu ile hadithi ya jinsi Israeli walivyokuja Palestina kwa ahadi ya Mungu. Nasi twajua kwamba yule Yoshua mkuu ndiye aliyewagawia kila kabila sehemu yao.

⁴³ Na ni, hakika, kama tungekuwa na muda wa kama tangu sasa hadi thenashara usiku wa leo, kukaa katika somo hili tu, kuyaweka sawa mambo haya, kupata maana yake hasa; ambao, hatuna, kama tu dakika thelathini, arobaini. Kwa hiyo yatubidi tugonge yale mambo muhimu tu, tukitumaini kwamba Roho Mtakatifu, kwenu ninyi wasomaji wa Biblia, ataweka mengine yote moyoni mwako, tunaposonga mbele.

⁴⁴ Ulijua kwamba vile visehemu, jinsi Yoshua alivyowagawia, huko Palestina, vilitolewa kwa ufunuo? Na wale mama wa Kiebrania wa wale wazee, mtoto alipokuwa anatoka naye akiwa katika utungu wa kuzaa, kumzaa mtoto, alitamka sehemu ile hasa ambayo wale wazee wangekaa na kuwepo siku za mwisho.

⁴⁵ Zungumzia kuhusu kutiwa pumzi, Biblia hii ina pumzi ya Mungu! Haidhuru ni dogo jinsi gani, kila Andiko dogo lina maana sana katika Maandiko, katika ile—ile picha kuu. Yote, kila—kila Neno lina pumzi ya Mungu, na katika hilo huning'inia kikomo cha nafsi, kwani ni Neno la Mungu Asiyekufa na wa Milele.

⁴⁶ Na hata wale mama, wakati mtoto alipozaliwa naye akatoa sauti zao, aliwaweka mahali pao ambapo wangekuwa katika nchi ya ahadi, mamia ya miaka baadaye. Naye Yoshua, pasipo kujua hilo, hata hivyo kwa uvuvio ule ule aliwaweka barabara mahali walipopaswa kuwa.

⁴⁷ Naye Yoshua, akigawa, aligawa kisehemu cha Yuda, kama ukiangalia kwenye ramani, ni ule. . . kijiografia ni magharibi tu ya bahari iliyo wazi, maili chache kusini mwa Yerusalemu, mji mkuu. Na wakati Yuda alikuwa akipewa sehemu yake au sehemu yake, hasa, katika nchi, jimbo lake, tungeliita, ni ajabu, lakini mji huu mdogo hata haukutajwa, Bethlehemu. Hata hivyo ulikuwepo, kwa sababu Ibrahimu. . . Au, naamini ilikuwa Rebeka aliyezikwa mahali pale. Lakini lazima ulikuwa kijiji kidogo cha namna fulani, kwa sababu kama ukisoma Yoshua 5, utaona kwamba kulikuwa na miji mikubwa maarufu mia moja na kumi na tano chini ya milki ya Yuda, mbali na vijiji na miji midogo; miji mikubwa mia moja na kumi na tano, iliyotajwa. Na labda wakati ilipogawanywa, basi Bethlehemu ulikuwa mdogo sana, labda tu nyu—nyumba moja ndogo au mbili, hata haukutajwa katika urithi. Ndipo tunaona kwamba kamwe haukujulikana. . .

⁴⁸ Mwazilishi wake alikuwa mwana wa Kaleb, mwana wa Kaleb, jina lake Salma, ndiye aliyeanzisha. Biblia ilisema alikuwa baba ya huo, ambalo linamaanisha alikuwa mwanzilishi wa Bethlehem. Kwa maneno mengine, lazima alihamia mle na kuanzisha biashara ya namna fulani, huo uchumi, na kufanya biashara, na kadhalika, ambazo ziliustawisha. Na baadaye tutaona kwamba sababu yake hasa, kwamba nchi zote zilikionea kijicho hicho kishemu kidogo cha nchi; ambacho kiko kaskazini, na mashariki, na kinateremka kidogo upande wa kusini, umbavuni mwa kilima. Nao ndio ulikuwa na rutuba sana katika Palestina nzima. Lilikuwa e—eneo la mahindi na eneo la ngano, na kulikuwa na mashamba makubwa ya mizeituni, na kadhalika, mle, katika sehemu hiyo ya Behtlehem, au Palestina, mwisho wa jimbo la Yuda.

⁴⁹ Na tunaona kwamba ulikuwa pia umefanyika makazi ya kahaba Rahabu. Wakati Israeli walipopita kwenye ukingo wa Mto Yordani, kuingia Palestina, tunafahamu hadithi ya kahaba Rahabu. Hebu tumwangelie asubuhi hii kwa dakika chache sasa, kama bi—bibi mdogo, kijana mwanamke mzuri, ambaye alilazimika kushikwa na bahati mbaya maishani, akiwa kafiri, alilazimika kuishi maisha yale aliyoishi. Na wakati mwingi watu wanalazimishwa kuishi maisha wanayoishi.

⁵⁰ Nilikuwa huko gereza usiku wa juzijuzi, kumwona mwanamume ambaye alikuwa akitumikia kifungo. Nami ni—nilimshika mkono, na kuzungumza naye. Basi nilisema, “Kwa nini utende jambo kama hilo?” Naye akinishika mkono, alianza kunena. Naye alilazimishwa kutenda alilokuwa akitenda. Nikasema, “Ni kwa sababu wewe uliruhusu hilo kukulazimisha kuingia katika jambo hilo. Si lazima ufanye hilo. Wewe, si lazima mtu kunywa pombe.” Nikasema, “Mimi nina wasiwasi, mimi mwenyewe, lakini hakuna haja ya hilo.”

⁵¹ Na kijana mwanamke huyu, baada ya kusikia kwake mara ya kwanza juu ya Israeli, na juu ya Mungu ambaye alikuwa Mu—Mungu ambaye alijibu maombi; si Mungu wa kumuomba tu, bali Mungu ambaye aliyejibu; aliposikia kwamba kuna Mungu wa miujiza, Ambaye angeweza kutenda miujiza, Ambaye alikausha bahari na kunyesha mikate toka mbinguni, moyo wake ulianza kutetemeka. Naye alipopata ujumbe wa kwanza kutoka kwa wahubiri wawili ambao walikwenda kule, upesi akaukubali kwa moyo wake wote. Na kulikuwa na kamba nyekundu iliyofungwa kwenye dirisha lake, kwa ulinzi wa nyumba yake, kwa sababu ameupokea ule ujumbe.

⁵² Nami ningeongezea hapa, umejua yeye alikuwa mfano wa Kanisa la Mataifa? Alikuwa Mtaifa, naye alikuwa mfano wa Kanisa la Mataifa, waliposikia ujumbe. Sote tulikuwa kwenye ukahaba wa kiroho, tukifanya uasherati wa kiroho dhidi ya Mungu wa Mbinguni, katika upuzi wa namna zote, namna zote za madhehebu na dini. Lakini tuliposikia kwamba kuna

Mungu ambaye angali hai, ambaye aliweza kutenda miujiza, upesi tukaupokea Ujumbe.

⁵³ Na hapo ikapakwa Damu ya Bwana Yesu, ambayo ilisababisha ile kamba nyekundu. Basi ili nisiisimulie kinaganaga, unajua jinsi ambavyo ilining'inia toka kwenye dirisha lake, hadharani, ile Damu ilionyeshwa hadharani. Hivyo ndivyo Damu inavyopaswa kuonyeshwa, hadharani, ikining'inia toka nje ya ukuta; kuonyesha kwamba, mle ndani, kitu fulani kimetendeka. Hiyo ndiyo namna mwamini wa kweli katika Kristo alivyo asubuhi hii; kwa nje ni onyesho la Damu ya Bwana Yesu, ambayo inaonyesha kitu fulani kimetendeka mle ndani.

⁵⁴ Na kupitia hii, Mungu aliangalia chini wakati ghadhabu iliposhuka na tarumbeta zikaanza kulia, Mungu aliona kamba ile nyekundu ikining'inia pale kama kumbukumbu. Sikuzote amempendeza Yeye kupita juu ya Damu. "Nitakapoiona ile Damu, nitapita juu yenu." Yeye aliiona. Na wakati mtetemeko na Roho Mtakatifu aliponguruma juu ya nchi na akazitikisa hizo kuta, zenye unene wa futi ishirini, hata jiwe moja halikuanguka mahali iliponing'inia ile kamba. Huonyesha ulinzi wa kweli wa Mungu kwa mwamini wa kweli, haidhuru una hali gani Yeye anapokuona, kama tu utakubali ile kamba nyekundu. Inapitia kote katika Biblia.

⁵⁵ Na kisha tunamwona alipokubalika kama mmoja wa Waisraeli. Alipendana na mwanamume, ambaye alikuwa kapiteni na mtawala katika Yuda. Alikuwa kapiteni, wa majeshi ya Israeli. Jina lake aliitwa Salmoni, kama tu yule mfalme, Sulemani. Basi alikuwa kapiteni naye huyu mwanamke akapendana sana na huyu kapiteni, ambaye alikuwa mtawala wa Yuda. Na hatimaye akaolewa naye. Na wakati mashamba yalipogawanywa kwa Waisraeli, yeye na mumewe mpenzi waliishi Bethlehemu.

⁵⁶ Sasa unaanza kuliona likifunguka, siyo? Unaona? Inaanza kufunguka tuonapo kwamba katika Bethlehemu yeye aliishi, akiwa bibi-arusi Mtaifa, kwa Myahudi. Kwa nini? Kwa sababu aliamini katika Mungu mwenye kutenda miujiza. Basi angalia alikotoka, kutoka kwenye nyumba ya sifa mbaya, ya ukahaba; kwa wongofu wake na kwa imani yake isiyoshindwa katika Mungu, ilimtoa toka nyumba ya ukahaba, hadi kwenye makazi mazuri huko Bethlehemu. Tofauti jinsi gani!

⁵⁷ Hivyo ndivyo inavyotufanya sisi sote. Toka nyumba ya kutokuamini na kuhangaika, hayo matendo ya uasherati, na kila kitu; hadi mahali, mahali petu katika Kristo, ambalo ni jambo la kupendeza sana. Kutoka ya dhihaka hadi ya fahari sana, hiyo ndiyo tofauti iliyopo katika kuongoka kwetu. Na umeona, aliolewa na mtawala wa nyumba ya Yuda, kapiteni? Kapiteni huyo alimwakilisha Kristo, alijitwalia Bibi-arusi Mtaifa. Toka iliyo duni kwelikweli, kufikia cheo kikuu kabisa na mahali pazuri

sana nchini, kama tutakavyoifikia baadaye katika Ujumbe wetu, kuthibitisha kwamba hakingekuwa kitu kingine ila hicho. Ni mfano wa Kanisa la Kimataifa.

⁵⁸ Na tunaona kwamba wao walikuwa na makazi ya kupendeza huko Bethlehemu, yaliyo—yaliojengwa na Salmoni, na pangekuwa mahali mashuhuri, na mashamba yenye rutuba. Basi ni vizuri jinsi gani kufikiria juu ya nchi hiyo mashuhuri ya ngano pale, kwamba ingekuwa mahali pa mkate wa ulimwengu. Na, ni kweli, si ajabu ilimpasa Yesu kuzaliwa pale, kwa sababu Yeye alikuwa Mkate wa Uzima! Hapo ndipo mataifa yote yalikwenda kuchukua ngano yao, matatifa yote yalikwenda kuchukua mahindi yao. Kwani, ilikuwa kule Bethlehemu, ambako kulikuwa na hayo mashamba yenye rutuba. Na, unaona, kitu hicho kidogo, kusema tu, “Lo, lilikuwa jimbo la ngano,” bali hilo lilimaanisha jambo fulani. Na unaona jinsi yule mtawala wa Kimataifa, ama huyu mtawala wa Kiyahudi akichukua bibi-arusi Wake Mmataifa kumrudisha Bethlehemu, akakae mle, mahali pa kuishi, ambapo palikuwa na wingi wa mikate.

⁵⁹ Tunaona, kwa mapenzi haya makuu na utii mkuu kwa imani, kwa kahaba Rahabu, alimzalia Salmoni mtoto wa kiume, jina lake Boazi. Na sote tunafahamu hadithi ile nyingine kuu inayofungamana na hii hapa sasa. Basi Boazi alizaliwa Bethlehemu, kwa Salmoni na yule kahaba Rahabu.

⁶⁰ Na tuna...twaona kwamba miaka mingi baadaye, baada ya Naomi kuondoka nchini na kwenda kuishi pamoja na Wamoabu, na wakati walipokuwa wamemtendea mabaya naye alikuwa ametoka katika ushirika pamoja na waamini wengine, naye alijihusisha katika hali ya kurudi nyuma, katika nchi nyingine, miongoni mwa watu wengine. Kwa namna nyingine, alikuwa ameacha Kanisa la kweli linaloamini, kwenda katika ulimwengu kwa kitambo kidogo, kujiunga na kanisa la kirafiki, ambamo waliamini eti kila kitu ni sawa. Mle ndani, akampoteza mumewe.

⁶¹ Na si lazima iwe kila wakati katika kifo cha kimwili. Waweza umpoteze katika kifo cha kiroho, au umpoteze mkeo. Yakupasa kujiweka imara! Yakupasa kukaa ambapo unajua umefunikwa na ile Damu, haidhuru wengine wanaonekanaje, ni wakubwa jinsi gani, jinsi ilivyo mizuri minara waliyo nayo kwenye makanisa yao, au jinsi hizo kengele kubwa zinavyolia. Yakupasa ukae ambapo Damu inafunika dhambi ya watu. Mwaweza mpotezane, na, zaidi ya yote, unaweza umpoteze Bwana Yesu nawe ufungiwe nje.

⁶² Na tunaona basi kwamba baada ya wanawe kwenda, aliwapoteza wote wawili, naye alirudi kwa sababu hapakuwa na roho ya ufufuo mjini, wakati ule.

⁶³ Loo, jinsi ningependa kutulia hapa kwa dakika chache! Jinsi ningependa kuanzia hilo papa hapa na kukuonyesheni! Bila

kujali ni makanisa mangapi kati yao yamerudi nyuma; kaeni chini ya Damu, hapo ndipo penye makao. Ndani au nje, juu au chini, kwa heri na shari, po pote pale, kaeni chini ya Damu. Bali Naomi, alifikiri ingefaa kwenda na kujiunga na kundi jingine, kwa sababu walikuwa na taabu, mkate wa kiroho—mkate haukuwepo. Na, lakini Mungu ataurudisha. “Nitawarudishia, asema Bwana.” Kaa katika shamba Huo unakotoka.

⁶⁴ Kwa hiyo tunaona kwamba alianza kutamani kurudi, kwa sababu walisema kwamba ufufuo mkubwa umetokea. Na kama ukiangalia, Naomi alirudi katika “majira ya shayiri,” ilisema Biblia, mnamo wakati wa mavuno; kwa maneno mengine wakati ufufuo mkuu unaendelea, tukilitumia kiroho. Alirudi mnamo majira yale. Hakuna kilichobakia; hakuwa na cho chote.

⁶⁵ Na Orpa, mmoja wa wake za wanawe, alipoona kile alipaswa kuacha, akiwa mfano wa kanisa la kisasa, “kama itanibidi kwenda huko, itanibidi kuachana na dansi zangu, itanibidi kuachana na anasa zangu, na sherehe zangu.” Basi akalia tu na kumbusu mama mkwewe, akarudi.

⁶⁶ Lakini picha nzuri ipo hapa, kulikuwa na mmoja aliyeitwa Ruthu, pamoja naye, mkwewe mwingine, ambaye tena alikuwa mfano wa Bibi-arusi Mtaifa, ambaye alimbusu mama mkwewe, akisema, “Nitaacha kila kitu. Ninakwenda pamoja nawe. Watu wako na wawe watu wangu. Mungu wako na awe Mungu wangu. Utakapofia, hapo nitakufa. Unapozikiwa, hapo nitazikwa.” Ndivyo hivyo. Hivyo ndivyo apendavyo Mungu. Si yule mwamini mkwamia mpakani tu, nusu; lakini kujitoa kikamifu kabisa kwa Ufalme wa Mungu. Akambusu.

⁶⁷ Na kwa hiyo Naomi akasema, kumshusha moyo, akasema, “Afadhali urudi kwa watu wako. Mimi ni mzee, na hakuna tena wana ndani yangu.” Na sheria ilikuwa kwamba ilimbidi angojee mwana. Basi akasema, “Basi hamna tena ndani yangu. Na kama ningempata mume, kisha nimzae mwana, ungekuwa mzee mno hata hungeolewa naye, kwa hiyo wewe urudi tu kwa watu wako.”

⁶⁸ Lakini Ruthu alisema, “Sitarudi!” Imani, yenye shina, yenye msingi, imani kamilifu imekuja katika moyo wa Ruthu. Akasema, “Naenda moja kwa moja pamoja nawe.” Naye akaambatana naye, akamshikilia. “Nitakuwepo utakapokuwa.” Napenda hilo.

⁶⁹ Nasi tunafahamu jinsi hadithi hiyo inavyoendelea, kwamba huyu Boazi mkuu, ambaye alikuwa bwana wa mavuno, alikuwa kwenye mavuno wakati ule, naye alikuwa jamaa aliye karibu wa Naomi. Naye alipomwona Ruthu huko kwenye kazi dogo, akiokota masazo, kila jani dogo aliloweza kuokota, ambalo lilikuwa na ngano, alilishikilia, kwani lilikuwa ni uhai. Naye Boazi, akiwa ndiye bwana wa mavuno, aliagiza kwamba wavunaji wake waache matita machache mara kwa mara, kwa

ajili yake; naye angeyaokota, na kwa furaha. Na kisha akajaza lesu nzima kwake, siku ile. Na wakati Boazi, bwana wa mavuno, alipotoka na kumwalia Ruthu, na kuona uaminifu wake, akampenda.

⁷⁰ Mwangalie Boazi akimuwakilisha Kristo. Alikuwa wapi? Bethlehemu. Ruthu alikuja wapi? Bethlehemu. Alikuwa akipuria wapi? Bethlehemu. Angalia maana zote zile za kiroho kwa hili hapa, msingi wa tukio hili kuu linalotendeka, Mungu akilijua hilo hapo mwanzo?

⁷¹ Naye akaanza kumswali mkwewe, limpasalo kutenda. Na mwishowe Ruthu akaolewa na Boazi, Mtaifa ameolewa na mtawala tena, katika Yuda, na akakaa na kuishi katika Bethlehemu.

Ee, wewe Bethlehemu uliye mdogo, wewe hu mdogo miongoni mwa miji yote mkuu—ya Palestina; lakini imempendeza Mungu, ambaye kujua Kwake na matokeo Yake yamekuwa tangu zamami, tangu mwanzoni, ya kwamba Mwanae azaliwe pale.

⁷² Yeye anajua mambo yote, na Yeye hilitenda tu likawa sawa. Na hapo Ruthu akaolewa na Boazi. Na wakati Ruthu na Boazi walipooana; kama tungalikuwa na muda wa kuingia katika hiyo hadithi kubwa hapo, ambayo ni mojawapo wa matukio makuu ya mapenzi ya nyakati zote, wakati Ruthu na Boazi walipooana. Nanyi mnakumbuka. . .

Hebu na tusimame kwa dakika moja hapa. Ni nzuri mno kuipita!

⁷³ Ruthu alikuwa ni Mtaifa. Hakuwa na urithi kwa Myahudi, kama ambavyo sisi Mataifa hatukuwa na urithi. Kwa hiyo Naomi ndiye hasa ambaye angerithi. Kwa hiyo alikuwa amepoteza shamba lake la kwanza, vitu vyake vyote vilikuwa vimeuzwa kwenye mnada hadharani, kwa hiyo alikuwa. . . aliharimishwa, naye akaenda zake.

⁷⁴ Sasa aliporudi, kulikuwa na mtu mmoja tu ambaye angeweza kuukomboa urithi wake uliopotea, huyo alikuwa mtu wa jamaa aliye karibu kabisa naye. Naye Boazi alijua hili, kwa hiyo ilimbidi afanye namna ya kumfanya msichana huyu Mtaifa kuwa mkewe. Na ilimpasa kufanya nini? Ilimlazimu kununua shamba lote la Naomi, ili kupata shamba hili, ambapo Ruthu alikuwa sehemu ya shamba la Naomi. Na mtu pekee ambaye angeweza kulinunua, ilibidi awe mtu ambaye ni jamaa wa karibu, mtu wa jamaa aliye karibu. Hiyo ndiyo sheria ya ukombozi.

⁷⁵ Na njia pekee ambayo Kristo angeweza kununua mali ya Israeli aliyerudi nyuma, ilikuwa ni kuwa Jamaa Aliye Karibu. Njia pekee Mungu angeweza kuikomboa jamii ya binadamu, Mungu Mwenyewe ilibidi afanyike mwili. Naye Yesu alikuwa Mungu aliyefanyika jamaa wa karibu kwa jamii ya binadamu.

Yeye alikuwa Imanueli. Yeye akawa jamaa wa karibu. Alitwaa si namna ya Malaika, lakini namna ya mtumwa, ambaye aliosha miguu na akaishi. Na mbweha walikuwa na matundu, na ndege wa angani walikuwa na viota, lakini Yeye hata hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Yeye alikula, alikunywa, aka—akalia, akachekeka, kama watu wengine tu. Naye alikuwa Mungu, si nabii. Yeye alikuwa Mungu, kwa sababu ilimbidi awe jamaa wa karibu kusudi aikomboa jamii ya binadamu iliyopotea. Kwa hiyo, Boazi, katika mfano huu mkuu kule Bethlehemu; angalia ambapo huyu Mtu wa Jamaa aliye Karibu alipozaliwa kwa ajili ya jamii ya binadamu, ilipaswa iwe hivyo.

⁷⁶ Na basi wakati huyu Boazi mkuu alipomkomboa, ilibidi aonyeshe hadharani kwamba amekomboa mali yake yote iliyopotea. Kwa hiyo alikwenda kwenye lango la Bethlehemu, mji ule mdogo tena, basi akawaita wazee wa mji, naye akawajulisha kwamba siku ile amekwisha nunua kila kitu ambacho... Naomi alikuwa amepoteza. Kila kitu ambacho alipoteza, alikinunua. Naye akavitoea viatu vyake na kuvitupa mbele ya watu, kama ishara, “Na kama kuna mtu ye yote aliye na sababu ya kusema jambo fulani, aliseme sasa, kwani hii ni kumbukumbu kwamba nimekomboa kila kitu alichopoteza.”

⁷⁷ Loo, Jina la Bwana libarikiwe! Na Mtu wa Jamaa yetu aliye Karibu alipokuja, Yesu wa Nazareti, aliyezaliwa Bethlehemu, alisimama juu ya Golgotha, nao wakamwinua juu katikati ya Mbingu na nchi, kama kumbukumbu kwamba Yeye amekwisha komboa kila kitu ambacho jamii ya binadamu imepoteza katika kule kuanguka. Mtu anawezaje kudharau uponyaji wa Kiungu na nguvu za kufufuka kwa Bwana Yesu, wakati ishara ya hadharani ilifanyika hapo Kalvari, kwamba, “Nimekomboa jamii yote ya binadamu na kila kitu ambacho wamewahi kupoteza,” alikomboa nafsi zetu, akakomboa miili yetu, akakomboa kila kitu ambacho tulipoteza katika kule kuanguka. Mkombozi wetu wa Jamaa alikuja akafanyika mwili, naye akakaa kati yetu, naye akatoa ishara, akasema, “Imekwisha.” Nini imekwisha? Kila kitu kimekwisha. Tunakwenda moja kwa moja katika urithi wetu. Na kadiri siku zinavyoendelea, ndivyo tunavyozidi kukaribia.

⁷⁸ Boazi na Naomi... Baada ya kuoana kwa muda, walimzaa mwana, jambo ambalo lilizidisha ukoo, na huyo alikuwa Obedi. Naye pia akamzaa mwanawe, ambaye aliitwa Yese. Naye Yese alikuwa na wavulana wanane.

⁷⁹ Basi nabii mkuu Samueli ndiye aliyekuja na chupa ya mafuta, nabii mkuu aliyekwenda kwa Yese, na kusema, “Mungu amemchagua mmojawapo wa wanao kutawala na kuwatumikia watu Wangu.” Na ilikuwa kule nje upande wa nyuma kondeni, kule malishoni, ambako yule mvulana mdogo mwekundu, alikotolewa yule kijana mwembamba, Daudi, yule mzee... mdogo kuliko wote. Naye Samueli alimminia mafuta ya

kutia, mbele ya ndugu zake wote, na wale waliosimama karibu, naye akathibitisha kwamba Mungu amentia mafuta awe mfalme. Hilo lilitokea wapi? Bethlehemu. Atukuzwe Mungu Juu Mbinguni! Si ajabu, Bethlehemu, ambapo alitiwa mafuta ili awe mfalme.

⁸⁰ Na ni katika Bethlehemu, ambako Daudi alizaliwa. Na Mwanawe mkuu, Yesu, pia ilibidi azaliwe Bethlehemu, kwa sababu kuna uhusiano wa karibu mno kati ya hao wawili, Baba na Mwanawe. Huyu Mwana mkuu hakuwa tu Mwana, Yeye alikuwa Shina na Mzao wa Daudi, hata Yeye alikuweko kabla ya Daudi, Yeye atakuweko baada ya Daudi, alikuweko milele, tangu milele na kuendelea. Bali kwa kimwili, na mambo yote kutimizwa, Yeye alikuwa Mwana wa Daudi. Yeye alikuwa azaliwe miaka mingi baadaye katika Bethlehemu ii hii, mji mdogo ulioachwa.

⁸¹ Bali wakati wote, ndani hapo, unaona, kunatendeka siri kubwa sana ambayo hakuna mtu aliyeonekana anaelewa. Ni kitu hicho hicho katika Bethlehemu ya Mungu leo, kunatendeka i—ishara ya siri, bali hakuna mtu aliyeonekana anaelewa. Ni kitu kinachopita juu ya vichwa vya watu. Hawaonekani wanakipata. Haidhuru ifanywe nini, au isemwe nini, na sehemu ya siri ya mambo ambayo yamefanyika, watu watasema, “Loo, vema, nafikiri ni sawa,” na kuendelea na mambo yao, lakini hawaelewi. Hawawezi kulishika. Hawawezi kulifahamu lote. Basi hilo ndilo Mungu alikuwa akifanya katika Bethlehemu ya Yuda. Yeye anatenda kazi, mambo yote haya madogo yakitendeka, kufikia kichwa kikuu kimoja.

⁸² Daudi, loo, alipotiwa mafuta ili awe mfalme, kama m—mvulana mdogo, alikuwa mwekundu ukimwangelia, bali lazima alikuwa na kitu fulani ndani yake ambacho kilionekana halisi kwa Mungu. Mtoto mdogo sana, kitinda mimba cha jamii. Wavulana wengine, watu wakubwa wazuri, wangeonekana wa kupendeza wakivaa hayo mavazi, na taji vichwani mwao. Lakini Mungu alionyesha ambacho Yeye anaangalia; si yaliyo mbele ya macho, lakini ndani ya mtu. Yeye aliutazama moyo wake, Naye akajua kilichokuwa moyoni mwa Daudi, haidhuru jinsi gani taji ile ingeonekanaje kichwani mwake. Yeye alijua alikuwa anajitafutia mtu ambaye alikuwa mtu ampendezaye, binafsi, ambapo Daudi angekuwa mtu ampendezaye. Hiyo ndiyo sababu Yeye alimmiminia hayo mafuta ya kutia, au aliagiza yamiminwe juu ya Daudi. Ambalo, jina *Daudi* humaanisha “mpendwa.”

⁸³ Na lilikuwa limewakilishwa vizuri katika Yesu, yule Mtu Mpendwa, miaka mingi baadaye; Mwana wa Daudi, Ambaye ilikuwa aje kutimiza mambo yote ambayo yamekwisha ahidiwa. Mji huu mdogo wa Bethlehemu ndipo ambapo hili lilifanyika. Na ilikuwa katika vilima vile vile vidogo vya Yuda ambapo Daudi alichunga kondoo wake, miaka mingi baadaye, ambako wale Malaika waliimba noeli yao ya kwanza kwenye vilima

vya Yuda, wakiangalia Bethlehemu. Noel ya kwanza, “Kwa ajili yenu amezaliwa katika mji wa Daudi, Kristo Bwana.” Wakati Malaika walipojitokeza mara ya kwanza kuimba, haikuwa huko Yerusalemu, lile kanisa kubwa; wala haikuwa huko Gilgali; au wala haikuwa huko Shilo, ambako walikuwa wanafanya ibada za kimadhehebu ya kidini wakati wote. Lakini ilikuwa katika Bethlehemu ulio mdogo, ambapo Roho wa Mungu alikuwa akitenda kazi kwa njia ya siri, akileta kitu fulani. Ilikuwa huko.

⁸⁴ Huko ndiko Kristo alipaswa kuja. Huko ndiko. Ilikuwa papo hapo katika mji ule ule mdogo, akazaliwa Mfalme, ambamo mama, bikira, alimzaa mwanawe wa kwanza. Ulimkinga, na kufanyia makao katika ngome yake ndogo, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. Haikuwa tu kwamba Samueli alikuja kumimina mafuta ya kupaka, lakini Mungu alimmiminia juu yake, na juu ya ulimwengu, Kristo Bwana. Malaika walitangaza kuja Kwake na wakawaimbia wachungaji kwenye mtelemko wa kilima, ambao walimfuata mfalme Daudi, miaka mingi kabla. Unaona siri ya Mungu, jinsi ilivyo kuu?

⁸⁵ Alizaliwa katika eneo hili kubwa la ngano, ambapo kutokana na ngano moja huja misingi ya kwanza ya uhai. Naye alikuwa Mkate wa Uzima. “Mimi Ndimi Mkate wa Uzima. Yeye alaye mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu yuna Uzima wa Milele, naye hatakuwa kamwe au kuingia hukumuni, lakini amepita toka mautini kuingia Uzimani.”

⁸⁶ Bethlehemu! Jina beth-el. B-e-t-h, beth, *beth* katika neno la Kiebrania humaanisha “nyumba.” *E-l* humaanisha Elohim, mkato wake, *Elohim* maana yake ni “Mungu.” B-e-t-h, beth; E-1, E-1 ni Elohim, ambalo ni Mungu, Nyumba ya Mungu, ambapo Mkate wa Uzima unawekwa. E-1, h-e-m, limalizie na uirudishe 1 yako na e yako, humaanisha “mkate wa bofulo,” katika Kiebrania, El-hem. E-1 ni Mungu, Elohim. B-e-t-h ni mkate, au b-e-t-h ni . . . b-e-t-h ni “nyumba”. E-1, ni Elohim, mkato Kisha E-1, he-m ni “mkate.” Alikuwa nini? Nyumba ya Mkate wa Mungu. “Nyumba ya Mkate wa Mungu.” Nyumba, *beth*; *Elohim*, Mungu; *El-he-m*, mkate. “Nyumba ya Mkate wa Mungu,” humaanisha *Bethlehemu*.

⁸⁷ Yeye angezaliwa mahali pengine gani isipokuwa hapo? Bali ilifichwa kwa kila mtu isipokuwa yule nabii; alisema, “Kutoka Bethlehemu atakuja Yeye.” Walikuwa wakiangalia Yerusalemu; walikuwa wakiangalia katika Shilo mkubwa; walikuwa wakiangalia kila mahali. Lakini Yeye alikuja kutoka Bethlehemu, sababu ilikuwa Nyumba ya Mkate wa Uzima wa Mungu. Yeye ni kikapu cha mkate wa Mungu kwa ulimwengu. Huyu hapo, amezaliwa Bethlehemu. Asingeweza kuzaliwa mahali pengine po pote.

⁸⁸ Kungekuwa na mambo mengi makubwa, ambayo nilikuwa nikijifunza juma hili ya hali mbalimbali za kiroho kwenye jambo

hilo, kwa nini Yeye azaliwe Bethlehemu. Nilipogusia sehemu hizi chache, Roho Mtakatifu alininyakua tu, nami nikasema, “Ee Mungu, hilo latosha. Ninaliona sasa.”

⁸⁹ Asingeweza kuzaliwa mahali pengine isipokuwa Bethlehemu. Palikuwa mahali pa mkate wa taifa. Ulikuwa mkate wa nyumba yote ya Israeli, ulitoka hapo. Naye alikuwa Mkate wa Uzima ulioshuka toka Mbinguni, ile Mana ya rohani; yabidi itoke Bethlehemu, eneo la mkate, mahali palipo na mkate. Bethlehemu, kuokwa kwa mkate. Sasa, Yesu akiwa Mkate wa Uzima, “Mtu aweza kuula.” Yeye alisema, “na asife kamwe.”

⁹⁰ Tukio jingine kuu ambalo nisingesahau kulitaja, hiyo ilikuwa wakati Daudi alipokuwa katika wakati wake mbaya sana, alipokuwa mkimbizi. Alikuwa amekwisha tiwa mafuta, alijua alichopaswa kuwa. Alipaswa kuwa mfalme, Mungu alinena hivyo, na hata hivyo alichukiwa. Naye alikuwa amesimama katikati ya mioto miwili mikubwa na yenye kina kirefu; hapa walikuwako Wafilisti upande mmoja, wakimwandama, hapa alikuwepo Sauli kwa upande mwingine. Naye alikuwa mtu asiye na taifa.

⁹¹ Kama Kanisa linavyosimama leo, Kanisa la kweli lililo hai la Mungu, bila ya madhehebu au kitu cho chote kile. Linasimama peke yake, lakini hata hivyo Hilo limekuwa na upako uliomiminwa juu Yake. Linajua kile lilicho.

⁹² Lingewezekanaje ulimwenguni kutukia, Shetani akiwa pande zote mbili, akimfukuza Daudi? Alikuwa amekimbilia ngomeni huko nyikani na katika mapango, akijaribu kujificha, na kikundi kidogo cha mashujaa waaminifu, wachache tu wanaoamini kama yeye. Lakini watu hao walimwamini Mungu, kwamba huyo angekuwa mfalme.

⁹³ Hivyo ndivyo ilivyo kwa waamini leo, ambao wamefichwa mahali hadi mahali, bali hata hivyo wanajua ni Nani anakuja kuwa Mfalme. Sijali ni nani atakayekuwa Rais. Tunajua Yeye yuaja. Na inaonekana mbali zaidi kuliko ilivyowahi kuwa, wakati sayansi inajaribu kukanusha jambo hilo, na kusema, “Wanaweza kutengeneza mtu, wanaweza kufanya *hili*, nao wanamchukua sungura na kuchukua mbelewele na kutengeneza sungura mwingine, na kadhalika,” wakijaribu kulikanusha Neno la Mungu. Hata hivyo, kuna watu wanaomwamini Mungu, ambao wanasimama wima kama walivyowahi kufanya. Haidhuru kitu gani kinakuja au kwenda, bado wangali wanamwamini Mungu. Mungu yu sahihi! Wanashikilia mikono ya Mungu isiyobadilika. Katikati ya vita, katikati ya machozi, katikati ya maradhi na mauti, na kila kitu, bado wanashikilia mkono wa Mungu usiobadilika. Wanajua kwamba Yeye ndiye Mfalme anayekuja.

⁹⁴ Watu leo hucheka na kuwadhihaki, na kuwaita, “watakatifu wanaojifingirisha,” huwaita kila kitu wanachotaka kuwaita,

lakini hao mashujaa wa Mungu husimama waaminifu kwenye kituo chao cha kazi. Waweza wawaite, “kundi la waponyaji,” waweza kuwaita “kundi la washupavu wa dini,” au lo lote unalotaka kuwaita; wanamshikilia Mfalme yule. Wanajua yuaja katika nguvu. Ingawa huapa bure kwa Jina Lake, kumdhihaki na kuchekelea, kuwaita wale watu wanaomwamini Yeye, “kundi la wenye kutupwa, maji yaliyotupwa,” hilo haliwaudhi hata kidogo, wanadumu waaminifu kazini mwao.

⁹⁵ Nao mashujaa waliokuwa na Daudi, walikaa papo hapo karibu naye. Kama Mfilisti akija, ilimbidi apigane. Hata iwe nani, walivamiwa, kila upande. Maskini Daudi, akilini mwake, amechanganyikiwa sana; alifikiri, “Yawezejekana je, Bwana?”

⁹⁶ Unajua, viongozi wakati mwingine hupitia katika mambo ambayo kusanyiko hawajui wanachopitia. Unapofikiria ahadi alizofanya Mungu, basi kwa nini isitimie? Hawaliambii kusanyiko lao, hawawaambii watu wenzao, lakini kuna usumbufu mwingi katika moyo wa kiongozi halisi.

⁹⁷ Daudi akiketi pale, koo—koo lake limekauka sana, na ilikuwa katikati ya majira ya joto. Wafilisti walikuwa wanatumia utengano kati ya Daudi na Sauli. Naye Sauli alikuwa anamtafuta Daudi kila mahali, na Wafilisti, pia, na kisha Wafilisti wanawatafuta Waisraeli. Nena kuhusu muda wa kuchanganyikiwa; kama tu ilivyo hivi sasa. Daudi alikimbilia mahali hapa padogo, katika kibanda hiki kidogo, kila mahali alipoweza kufika, vijingome vidogovidogo ambavyo aliweza kushikilia. Kisha akapanda mlimani, kwenye yale majira ya joto, katikati ya majira ya kiangazi, wakati joto lilipokuwa kali sana, koo lake likimkaukia, na wasiwasi na woga moyoni mwake, huku anashangaa, “Ee Mungu, imekuwaje? Wewe ulinimiminia yale mafuta, si kwa sababu nilijichagua mimi mwenyewe, bali Wewe ulinichagua mimi. Mbona Wewe ukaniita kutoka kwenye kuwachunga kondoo nje huko, na kuniambia Wewe ungenipa jambo hili ili kuwatumikia watu Wako, na hapa uneniweka katikati ya mioto kila mahali?” Hayo yalikuwa yakipita moyoni mwake.

⁹⁸ Aliketi juu ya kilima na kutazama chini, na hapo Wafilisti walikuwa wamekuja na kutia ngome katika Bethlehemu, makazi yake madogo. Basi, mji wake mdogo ulikuwa chini ya utawala wa serikali ya adui. Si hilo tu, bali nyumba ya baba yake, nyumba ya Yese, ilikuwa chini ya utumwa wa Wafilisti. Hilo hapo taifa lake, kanisa lake, dhidi yake. Huyu hapa yule adui aliyekuwa anampiga vita, hawa hapa watu wa kanisa aliokuwa anapigana nao; sio kwa sababu alitaka, bali kwa sababu alilazimishwa kufanya jambo hilo.

⁹⁹ Na wakati mwingi tunashurutishwa kufanya mambo na kusema mambo ambayo hatutaki kuyasema, kiongozi halisi wa kiroho, bali anashurutishwa kulitenda. Yambidi achukue

msimamo wake na kuonyesha alivyo hasa. “Nitafuata njia pamoja na wachache wa Bwana wanaodharauliwa,” alinena mwandishi wa wimbo.

¹⁰⁰ Basi huyo hapo, kwenye siku yenye joto, bila shaka, akitembea huku na huko, akitazama chini kwenye bonde lile refu, la kama maili ishirini na tano chini kule, na kurudi. Nyumba ya baba yake mwenyewe ilikua katika—katika utumwa wa Wafilisti. Huyo hapo Sauli kule ng’ambo, ile...na hapa yuaja huyu, akiketi moja kwa moja katikati, unaona, awe upande wake. Akiona ule wakati mkuu ambapo Israeli walikuwa wametengana, kanisa limegawanyika katika madhehebu tofauti, tuseme. Huyu hapa Daudi amesimama nyuma huku, hajui la kufanya, na hata hivyo akijua kwamba ana upako juu yake. Wao walijua kwamba upako ulikuwapo. Wao walijua kwamba Daudi atakuwa mfalme. Haleluya!

¹⁰¹ Tunajua Ambaye atakuwa Mfalme. Haidhuru ni nani atakayekuwa Rais. Najua ni Nani atakayekuwa Mfalme. Yeye atakuwa Mfalme. Nami najua inahitaji kitu fulani kusimama. Bali Mungu na anisaidie kuyafumba macho yangu kwa madhehebu na cho chote kile, nipate kuangalia kwenye jambo lile la kiroho kule, kwamba Yeye ndiye Mfalme ajaye. Nitamtumikia Yeye. Kama ni mauti, hebu nife; kama ni jamaa yangu, ni wapenzi wangu, kama ni madhehebu yangu, ni kila kitu. Hebu na nimtumikie Yeye. Nitakaa Kwake. Hao ndio mashujaa wa Mungu, kama ilivyokuwa kwa Daudi, wameshika upanga wao, wakati wowote walipotembea. Hivyo ndivyo mashujaa wa Mungu wanavyotembea, tayari!

¹⁰² Adui husema, “Yakubidi unywe kidogo, ili uchanganyike na watu.”

¹⁰³ “Sitagusa kitu hicho chenu kichafu.” Amina! Huyo hapo adui. Huyo hapo shujaa Wake!

¹⁰⁴ “Loo, hivi kwa nini usikanushe upuzi huo wa kale unaoamini wa watakatifu wanaojifingirisha?”

¹⁰⁵ “Nitamwamini Mungu. Nitakuwa wa kweli!” Naam basi. Hao ndio wale mashujaa.

“Loo, kumbe? Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu!”

“Hilo ndilo unalofikiria. Najua vizuri zaidi.” Unaona?

¹⁰⁶ “Hakuna kitu kama Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hizo siku zimeisha pita.”

¹⁰⁷ “Hilo ndilo unafikiria. Nimekwisha Upokea, umechelewa sana kuniambia cho chote kuhusu jambo hilo.”

¹⁰⁸ Walijua upako ulikuwepo juu ya maskini jamaa yule mwekundu, nao walijua atakuwa mfalme.

¹⁰⁹ Lakini Daudi, niani mwake, alikuwa amefadhaika. Naweza kuwazia, hebu mwangalie kwa dakika moja, anarudi nje kule

na kuketi chini, anaangalia chini kule, na kuwaza, “Mji wangu niupendao, Bethlehemu, hebu uangalie pale, ambako mambo makuu ya Mungu yametukia, ambako baba wa baba wa baba wa baba yangu alizaliwa; ambapo nyanya wa nyanya wa nyanya wa nyanya yangu huko alitamka katika, katika wakati wa kuzaliwa kwake Yuda, kabila ambamo ninatoka. Lakini huko kulikuwa na kitu kisicho cha kawaida. Alitamka mahali pao, na hapo Yoshua akaliweka; mwana akiwa ndani yake. Na kupitia hapo yakaja mambo yote haya hapa. Yapaswa kuwa hivyo. Nilikuwa mchungaji wa kondoo, Nawe ukamimina mafuta juu ya kichwa changu. Ulisema ningekuwa mfalme. Ninakuamini. Amina.”

¹¹⁰ Kisha anarudi na kuangalia chini kule, na kufikiri, “Vema, chini mbali huko katika mji wangu mdogo, nilikozaliwa, kundi lile dogo nililokuwa pamoja nao, hizo siku nzuri za kale.”

¹¹¹ Ingefaa kama Wamethodisti wangeangalia nyuma kwenye siku zao njema za kale, walipokuwa wachache na wako mbali huko na huko katika nyumba ndogo za shule humu Marekani, wakianguka chini ya Uweza wa Mungu, wakijitupia maji usoni mwao. Ingefaa kwenu ninyi Wabaptisti kutazama nyuma ambako mlitoka, pia, na wale wengine wote. Ninyi Wapentekoste, angalieni mnakotoka. Hilo ni kweli.

¹¹² Vita vilipowaka moto hapa, Daudi akaanza kuwaza, “Loo, naweza kukumbuka siku zile nilipolala kule kwenye mtelemko wa kilima. Nakumbuka nilipoziangalia nyota, jinsi zilivyosogea juu kule, na jinsi ambavyo Mungu alivyozungumza na maskini moyo wangu wa ujana. Naweza kukumbuka nilipoingia sana katika Roho, siku moja, nikiyaangalia mawingu na malisho yenye vivuli ya majani mabichi, mpaka nikapaza sauti katika Roho, na nikaimba.

BWANA ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu

Naam, nijapopita kati ya bonde la vivuli vya mauti, Sitaogopa mabaya; Kwa maana wewe upo pamoja nami, . . .

¹¹³ Loo, jamani, huyu hapa katikati ya taya za mauti saa hiyo hiyo, pande zote mbili. “‘Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti.’ Siku hizo nzuri za kale wakati Roho alipokuwa pamoja nami, Mungu alipokuwa pamoja nami; niliimba sifa Zake, nilimfurahia Yeye.

¹¹⁴ “Ninakumbuka wakati mmoja simba alipotokea asubuhi moja, na akamchukua mmoja wa kondoo zangu. Na Roho wa Mungu akaja juu yangu, nami nilitoka nikamkamata na kumkata vipande vipande. Nakumbuka ukombozi huo. Loo, naweza kukumbuka jioni ile kabla tu ya jua kuchwa, dubu alikuja na akamshika mmoja, nami nikamuua. Ukombozi mkuu huo!

¹¹⁵ “Ninakumbuka nilipoimba sifa Zake katika siku za utoto wangu, nilipochunga kondoo zangu. Ee Mungu, nirudishe mahali hapo. Nirudishe kwenye upendo wangu wa kwanza. Nirudishe na unirudishie fimbo yangu ya mchungaji. Nirudishie kundi langu la kondoo. Nijalie nikae peke yangu nyuma kule, kukuabudu Wewe.”

¹¹⁶ Hilo, wakati mwingine tunafikiria hilo, lakini tuko kwenye vita vikali. Jambo fulani lapaswa kutendwa. Tulikuwa vijana wakati mmoja; sasa tu watu wazima. Vita vimewaka moto. Nakumbuka wakati unga wa mbao ulipochemka sakafuni, na watu wakipiga makelele na kupaza sauti nawe usingeweza kwenda mahali po pote hapo, kwa wingi wa watu, bali sivyo ilivyo leo. Vita vimewaka moto. Loo, si William Branham, yule maskini mhubiri mdogo, tena; yakupasa ufanye jambo fulani, ndiyo, bwana, yapaswa kuwe na kitu cha tofauti. Wakati umewadia. Vita vimewaka moto. Kumejaa joto. Wakati wa kukombolewa, watu, kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kile Kitabu. Sasa wakati umewadia.

¹¹⁷ Daudi na kuburugika kwake kwote, akitembea huku na huko, na kuwaza, “Loo, siku hii yenye joto! Whiu, loo, ni joto sana! Loo, huenda Sauli akatokea *huku*, Wafilisti watokee *huku*; majeshi yako kila mahali, na sisi hapa tumeketi kwenye mlango wa pango! Na, isitoshe, upako uko juu yangu. Imekuwaje, Ee Mungu, imekuwaje? Loo, laiti ningepata maji ninywe!” Ndipo akili zake zinarudi nyuma, chini huko kwenye malango ya Bethlehemu, palikuwa na kisima. Hamna maji kama maji hayo.

¹¹⁸ Wajua, baadhi ya maji ya Palestina ni mabaya. Wana maji machafu, na hata wana malaria kali, na ghasia, mle ndani. Na baadhi yake ni maji ya magadi ambayo yangekuua.

¹¹⁹ Lakini Bethlehemu ni makao makuu ya maji ya hilo jimbo, pia. Hapakuwa na maji kama uliyokuwa nayo Bethlehemu! Daudi alikuwa akiwaza, “Nichukuapo kondoo zangu na kuanza kutoka nao asubuhi, ningepita karibu ya kisima kile cha kale na kunywa.” Loo, jinsi yalivyo na baridi na jinsi yalivyo matamu, na jinsi yalivyozima kiu!

¹²⁰ Sasa koo lake laenda, linatiwa mafuta, “Loo, laiti ningepata kinywaji cha maji!” Sasa mashujaa wake...Naye akapaza sauti, katika kukata tamaa kwake, “Loo, laiti mtu angeniletea kinywaji tena kutoka kisima kile cha kale kule Bethlehemu!” Loo, baada ya kuota juu ya siku zake zote za ujana wake na ushindi, na kumuona katika mahali anapoketi hapa kati ya mioto, akapaza sauti, “Loo, laiti mtu fulani angeniletea maji kutoka Bethlehemu!”

¹²¹ Sasa, mashujaa wake hawakuweza kufasiri mawazo yake, lakini, ndugu, walimpenda kwa yote yaliyokuwa ndani yao. Hamu yake iliyo ndogo sana ilikuwa amri kwao. Watatu kati ya mashujaa wake wenye nguvu wakavuta panga zao,

wakaponyoka kutoka mle kambini, na wakafanyiza njia kwa kuwafyeka hao, maili ishirini na tano. Daudi, katika kuondoka kwao, bila shaka alishangaa, “Wako wapi? Wamefanya nini? Wamekwenda wapi? Walijua wanahatarisha maisha yao?” Wako katikati ya mataya ya mauti, kupitia mstari wa maili ishirini na tano, wameotewa kila mahali, na panga zikimetameta, na ngao zikivuma; bali mtu wao, ndugu yao ambaye waliamini kwamba angekuwa mfalme, alitamani kunywa maji.

¹²² Loo, ndugu, nashangaa kama mashujaa wa leo wako tayari kufanyiza njia katika desturi, shaka na kutokuamini, kuburudika katika Uwepo wa Bwana, hamu Zake? “Hamu Yako iliyo ndogo sana; kama ni Afrika, India, kama ni kwenda mitaani, po pote pale! Hamu Yako iliyo ndogo sana, Bwana, ni amri kwangu. Mauti hayamaanishi chochote kwangu. Kupendwa na watu, jamani. . . ? . . . , lile nitakalokuwa, halimaanishi kitu, Bwana. Ni kutimiza hamu Zako.” Hao ndio mashujaa wasimamao upande Wake. “Wakiniita ‘mtakatifu ajifingirishaye,’ kama wakilikashifu jina langu, kama wakinipiga teke mitaani, hilo si kitu. Hamu Yako ni amri kwangu.” Huyu ndiye askari halisi.

¹²³ Walifanya nini? Walienda zao wakipigana hata wakafika kwenye kile kisima. Wakatumbukiza ndoo na kuchota maji. Nao hawa hapa wanarudi, wakipigana, wakifanyiza njia kwa kuwafyeka kulia kushoto, huku wanakuja mbele za Daudi. Wakasema, “Haya hapa, bwana wangu!” Loo, jamani! Ni nini? Mtu ambaye alitahayarishwa, mtu ambaye alichukiwa na kanisa, mtu ambaye alichukiwa na mfalme, mtu ambaye alichukiwa na Wafilisti, mtu ambaye alichukiwa karibu kila mahali. Bali kundi dogo lilimfuata, walijua kwamba ndiye mfalme ajaye.

¹²⁴ Leo hii, najua tunaimba nyimbo kuu, tunajenga makanisa makubwa, tuna nyimbo nzuri sana na kila kitu, tunamsifu Yeye namna hiyo, lakini Yesu alisema, “Mioyoni mwenu mko mbali nami, kwani mwafundisha Mafundisho yaliyo maagizo ya binadamu.” Hebu Roho Mtakatifu aingie ndani na atende jambo katika kanisa lao, akionyesha Uwepo wa Yesu Kristo, watakupiga teke wakufukuze mle. “Wananiabudu Mimi bure. Wanaabudu, lakini mnafanya hilo bure, mkifundisha Mafundisho yaliyo desturi za binadamu.”

¹²⁵ Bali kuna mashujaa wanaomuamini Yeye, kuna mashujaa wasimamao kwa Hilo, wenye ufahamu wa kiroho, kama huko Bethlehemu mdogo. Unaona? Hakika, ilikuwa hivyo.

¹²⁶ Daudi akatwaa ndoo hii ya maji, akayaangalia, na Biblia inasema kwamba aliyamwaga ardhini, kasema, “Hasha Bwana, nisingekunywa hayo, kwa sababu hawa mashujaa wangu—wako wameyahatarisha maisha yao, kwenda huko na kuniletea mimi maji haya. Ni damu ya mtu. Siwezi kufanya hilo.” Ni

maji haya matamu ambayo wamejihatarishia maisha yao na kupenya katika mstari wa adui kwenda huko kuyateka, Daudi aliyamwaga ardhini kama sadaka ya hiari kwa Bwana. Haikuwa uchoyo, ilikuwa tu kutimiza Maandiko.

¹²⁷ Kwa sababu, ingawa Yesu, toka Bethlehemu, ni Mkate wa Uzima, Yeye pia ni Maji ya Uzima. Hakika, ndivyo. Na Yeye alifanya nini? Yeye alikuwa amewakilishwa katika Daudi na hao mashujaa pia; kwa sababu Yeye alikuwa Mfalme, pia alikuwa yule shujaa Ambaye alikuja na kupenya katika boma ya adui. Amina! Alishinda mauti, kuzimu, na kaburi, akamwaga Damu Yake Mwenyewe, ili Yohana 3:16 itimizwe!

*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu,
hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu
amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa Milele.*

¹²⁸ Na hivyo Yeye hakutoa maji ambayo yaliliwakilisha jambo hilo, bali Yeye alikuwa yale Maji, au upotee; watu wenye kupotea, ili wawe na Uzima. Alifanyaje jambo hilo? Kwa Damu Yake Mwenyewe, kwa kuimwaga; siyo kuimwaga Hiyo, kama kwamba ni ajali. Yeye aliimwaga Hiyo bure hapo Kalvari, baada ya Yeye kuvunja kila mstari wa adui, naye akaumwaga Uhai wa Damu Yake ili Yeye aweze kuwa riziki kwa ulimwengu.

Na Damu imebubujika,
Ni ya Imanueli,
Wakioga wenye taka,
husafiwa kweli.

¹²⁹ Hiyo ndiyo sababu Yeye alizaliwa Bethlehemu. Hiyo ndiyo sababu ilimbidi aje, kwa sababu ulikuwa ndio soko la mkate, Mkate wa Uzima. Ulikuwa soko la maji, hasa, Maji ya Uzima? Na katika Yesu mlikuwamo vyote viwili Mkate wa Uzima na Maji ya Uzima, kwa hiyo Yeye alipaswa aje azaliwe Bethlehemu.

Nawe Bethlehemu, wa Yuda, hu mdogo katika hao majumbe wote? U mhubiri mdogo tu wa kawaida, u kijitu kidogo tu; lakini kwako atatoka Mtawala ambaye ni wa tangu zamani, na tangu milele hata milele, matokeo Yake yamekuwa tangu zamani, na tangu milele hata milele.

¹³⁰ Hiyo ndiyo sababu yeye alizaliwa katika Bethlehemu wa Yuda. Ulimlea Yeye. Na, ndugu yangu, mahali anapotaka kulazwa leo ni katika nafsi yako, moyo wako, ili Yeye aweze kujidhihirisha ndani yako, Maji ya Uzima kwa watu wanaopotea, na Mkate wa Uzima kwa watu wanaokufa njaa. Yeye ni Mkate na Maji ya Uzima, ambayo ni mambo mawili ya lazima kwa maisha ya binadamu, ni mkate na maji. Imeahidiwa, hakika.

¹³¹ Hebu tuinamishe vichwa vyetu kidogo, na, katika kufanya hivyo, nataka mnisikize kwa makini sana. Umeishawahi

kwenda Bethlehemu, asubuhi hii? Kama hujawahi kwenda Bethlehemu...

¹³² Uliitwa Bethlehemu Efrata, pia, Bethlehemu *Efrata*. Efrata humaanisha “shina,” inatoka kwenye neno h-e-m-p, *hemp* humaanisha “shina.” Na ile wilaya ya zamani pale iliitwa Efrata, ambayo humaanisha, “ni mwanzo wa uhai.” Na Kristo alisema, “Mkikaa ndani Yangu, Mimi ni mzabibu ninyi ni matawi.” Yeye ni Shina la Uhai wote.

¹³³ Kama hujawahi kuja Bethlehemu Efrata, ile Bethlehemu, njoo asubuhi hii na umpokee kama Mwokozi wako, Naye atakusamehe dhambi zako. Utamnyooshea Yeye mikono yako, ukaseme, “Bwana Mungu, nihurumie sasa, sasa hapa naja kwa Yesu, kwa moyo wangu wote. Naja kwenye Bethlehemu Yako, kwenye Maji na Mkate wa Uzima. Sasa namkubali Yeye kama Mwokozi wangu binafsi?” Bwana akubariki, kijana nyuma kule. Bwana akubariki. Mungu akubariki, kijana mdogo.

¹³⁴ Kuna mwingine, aseme, “Sasa naja; sina cha mikononi. Nasimama, nikiona kiu, koo langu limekauka. Ninashangaa niende wapi ili nipate Maisha ya kweli. Ninashangaa. Nimejiunga na makanisa...” Mungu akubariki, dada. “Nimejiunga na makanisa, nimefanya kila kitu nijuacho kufanya, Ndugu Branham, bali kamwe sijagusa chemchemi ile ya kweli itoayo Uzima. Sasa naja, Bwana, kuupokea Huo.” Yeye yupo hapa kwa ajili yako. Hebu inua tu mkono wako, useme, “Ni mimi, Bwana. Ni mimi ambaye ninasimama, na nina haja?” Bwana awabariki, tunapoomba.

¹³⁵ Ee Bwana Mungu, huu ujumbe mdogo uliokatika-katika uliotolewa kwenye Maandiko, hata hivyo, katika mifano yake yote, ambayo Wewe uliweka mle; pengine imefichwa machoni pa wenye hekima na wenye akili, na kufunuliwa kwa watoto wachanga ambao watajifunza. Jinsi Bethlehemu ule mdogo, mdogo zaidi ya yote! Nabii alisemaje hilo? “Hu mdogo miongoni mwa majumbe wote?” Bali ilimpendeza Mungu sana kuleta toka mahali pale padogo pasipojulikana, Mtawala wa Israeli. Bwana Mungu, kutoka katika kikundi kidogo cha watu ambao wameoshwa kwa Damu nyekundu na iliyo hai ya Bwana Yesu, Wewe utamleta, kwa kundi lile, mahali fulani, Bwana, kote katika ulimwengu huu, Kristo tena, ambaye atayatawala mataifa yote kwa fimbo ya chuma.

¹³⁶ Nakusihi Wewe, Baba Mungu, kwamba Wewe utamrehemu kila mmoja wetu aliye hapa sasa, na tujalie tuje Bethlehemu Yako. “Njooi kwa imani,” tumekuwa tukiimba, “njooi Bethlehemu upesi.” Na Bwana, hebu waone kwamba si kwenda kwenye kidogo kule, ambacho wakati mmoja kilikuwa katika mifano; lakini kwenda kwenye kitu halisi, Yesu Kristo, Mkate wa Mungu na Maji ya Uzima.

¹³⁷ Na hawa walioinua mikono yao, wapokee katika Ufalme Wako, sasa hivi, Bwana, kwani ni kwa imani yao wao—wanampokea Yeye, ni kwa imani kwamba waliinua mikono yao, na ni kwa imani kwamba ninaamini Wewe unawapokea. Wahifadhi, Bwana, hapo Bethlehemu, ambapo hawatapotea kamwe au kwenda zao kama Naomi; lakini waweze, kama majira yanakuwa magumu, hebu wakae papo hapo Bethlehemu. Itafaa, baadaye. Jalia jambo hilo, Bwana.

¹³⁸ Sasa naomba kwamba Wewe utawarehemu walio wagonjwa na wanaoteseka. Wapo wale hapa, Bwana, wanaohitaji mguso Wako wa uponyaji. Ee Bwana, Wewe ulirejesha Bethlehemu kwenye utukufu wake wote wa kwanza. Uliurejesha wakati wa huzuni, ulipokuwa mgonjwa. Uliurejesha moja kwa moja na ukamleta Naomi kwenye majira ya shayiri. Na sasa, Baba, tunaomba kwamba Wewe hata utamleta kila Naomi, na kila mmoja ambaye yumo humu ndani na ni mhitaji. Naomba, Mungu. Ee Bwana, ni majira ya shayiri, mkate ule mkuu wa shayiri ambao ulionekana, ukija unavingirika ukishuka kilimani, hadi kwenye kambi ya adui. Naomba, Mungu, kwamba Wewe utaleta ghala ile kubwa ya shayiri katika jengo hili sasa, na kwamba Hiyo iweze kuwa upatanisho kwa ma—magonjwa ya watu, na dhambi zao pia, na umponye kila mtu ambaye yupo katika Uwepo wa Kiungu.

¹³⁹ Najisikia tu, Bwana, huenda ikawa ni kuhisia kwangu mimi, lakini najisikia kwamba Wewe uko karibu, kuwako Kwako humu ndani sasa. Naamini kwamba Wewe upo hapa. Na sisemi hili kwa sababu ya watu; Wewe Ambaye unajua moyo wa binadamu. Naomba, Bwana, kwamba kwa namna fulani watashika lile ono, asubuhi hii, kama wale mashujaa, kwamba Uweza Wako mkuu, Nguvu Zako kuu, Uwepo Wako mkuu, jinsi Wewe ulivyo, Mwana wa Mungu, yule Mfalme, Yeye yule aliyetiwa mafuta, kwamba Wewe upo katikati yetu; watapata tazamo Lake la mara moja, nafsi mwao, na waponywe mateso yao. Naomba sala hii, ninapoiweka kwao, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana Wako. Amina.

¹⁴⁰ Ninamwamini Mungu, Maneno Yake yote, naamini kwamba kila sehemu ya Neno Lake limetiwa pumzi Kiungu. Naamini kwamba Yeye si “Nilikuwa,” bali Yeye ni “MIMI NIKO,” Uwepo ulio hai sikuzote. Naamini hilo sasa hivi, miongoni mwa watu hapa.

¹⁴¹ Ninyi mlioinua juu mikono yenu, jitafutieni kanisa, “mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo, mkimwitia Mungu, mkazisafishe dhambi zenu,” mkiamini kwamba kuja kwake kunakaribia... Yeye ataonekana katika Kuja Kwake kwa Mara ya Pili.

¹⁴² Ninaamini pia kwamba Uwepo Wake upo hapa kuwaponya wagonjwa, kuwafanya wazima wale walio wahitaji.

Haiwalazimu muombewe mmoja mmoja. Nilithibitisha hilo usiku wa juzijuzi, kwa watu, kwamba nilitaka tu kuwaonyesha ambacho kingetukia.

¹⁴³ Palikuwa na kijana fulani, ambaye anaketi, akiniangalia mimi moja kwa moja sasa hivi, ambaye alikuwa amelala kitandani kwa siku nyingi. Koo lake lilikuwa limevimba vibaya sana hata hakuweza kula wala cho chote, homa yake ilikuwa juu sana. Naye amewaambia baba yake na mama, “Tumaneni, mwambieni Ndugu Branham aje aniombee.” Na kwa namna fulani hawakutaka kunisumbua, sababu nilikuwa na shughuli nyingi. Na Kitu fulani kilinielegeza kwenda nyumbani kwao.

¹⁴⁴ Nilipokuwa nimeketi pale, walijaribu kumletea kijana yule sahani, ilikuwa na yai laini sana na kitu kingine, na maharage laini ya mseto, naye alikuwa akijaribu kuyameza. Angeyaseta kwa vidole vyake na kuyaponda, meno yake yote yalikuwa yamevimba na yakitokwa na usaha. Na—na angejaribu kuyaseta namna hiyo, kwa vidole vyake, na kujaribu kuyaingiza ndani ya koo lake namna hiyo. Naye akafanya yapata mego moja au mbili, naye hakuweza kuendelea, akayaondolea mbali.

¹⁴⁵ Nilikuwa nimeketi pale, bila ya maombi; kuna kitu kidogo, huwezi kumwambia kila mtu kinachoendelea. La. Nikasema, “Bwana, Bwana, ni karibu na mwisho wa mwaka sasa. Linakuja sasa, jambo jipya. Nijalie. Bwana, je, ndilo hili, ndilo hili?” Na mara nilipoanza kusema hilo, na kusema sasa, katika moyo wangu sasa, “Najua Wewe upo hapa,” huyo kijana akaunyosha mkono wake akapata mego nyingine, na mego nyingine, na mego nyingine, na mego nyingine, akamaliza sahani yake yote, akaingia kwenye gari lake akaenda zake.

¹⁴⁶ Loo, Yeye ni Mungu, unaona, Uwepo Wake, Uwepo Wake. Hawa . . . Inamwacha tu Yeye aweo.

¹⁴⁷ Hivi majuzi walipoipiga hii picha ya mwisho, picha ya hivi karibuni. Nilipomwona Yeye amesimama pale, niliangalia, na nikawaza, “Vema, nimemuona Malaika wa Bwana katika yale, na najua lilikuwa jambo la ajabu.” Bali Yeye alipopigwa hii! Kisha mnamo saa tisa usiku, Yeye aliniamsha na akanieleza itakavyokuwa, na akanieleza yote, na jinsi ambavyo silaha zote na kila kitu, akanionyesha mambo juu yake nisiyopata kuona. Niliingia na nikaichukua, na nikaiangalia, hiyo hapo basi. Sijawahi kuona hapo kabla. Loo, jinsi hilo lilivyoniletea hisi nzuri sana, faraja, kujua kwamba Yeye yupo!

¹⁴⁸ Yeye yuko hapa, Uwepo Wake tu. Na Uwepo wa Bwana ulikuwepo pale kuwaponya wagonjwa. Uwepo wa Bwana upo hapa kuwaponya wagonjwa. Uwepo wa Bwana upo hapa kuwaletea wenye dhambi thibitisho la makosa yao. Uwepo wa Bwana upo katikati ya watu Wake, na Yeye ni Bethlehemu ya Mungu, uliojaa Mikate na Maji. Ninafuraha sana (nanyi je?) kwamba tuna mahali pa kuja, kula na kuishi milele.

¹⁴⁹ Sasa Bwana awabariki. Una kitu unachotaka kusema, ndugu? [Ndugu Neville anasema, “La.”—Mh.] Tusimame kwa miguu yetu, kwa muda kidogo. Wimbo wetu wa zamani wa kuachana, “Peleka Jina la Yesu.”

¹⁵⁰ Ni wangapi wanampenda Bwana, hebu tuone mkiinua mikono yenu juu sana. Sasa wakati mmeinua juu mikono yenu, sasa ishusheni, na peaneni mikono na mtu anayesimama karibu yako, msemi, “Mungu na akubariki, msafiri. Mungu akubariki.” Sawa, halafu geukeni. Vema, hilo ni kusudi mfahamiane ninyi kwa ninyi. Sawa.

¹⁵¹ Sasa hebu na tuangalie moja kwa moja juu mbinguni na kuimba wimbo huu sasa.

Peleka Jina la Yesu,
Ko kote uendako;
Litafurahisha moyo,
Peleka uendako.

Thamani, (thamani) na tamu,
Ni Jina lake Yesu;
Thamani, (thamani) na tamu,
Ni Jina lake Yesu.
(Sasa kumbukeni . . .)



KWA NINI BETHLEHEMU MDOGO? SWA58-1228
(Why Little Bethlehem?)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Desemba 28, 1958, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1990 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org